BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>

<u>MKUTANO WA SABA</u>

<u>Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 16 Mei, 2022</u>
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

<u>Waziri wa Afya:</u>

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/2023.

<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:</u>

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka 2022/2023.

## II. <u>MASWALI:</u>

<u>Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:</u>

109. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

     Kwa kuwa uwepo wa barabara husaidia sana suala la usafiri wa abiria pamoja na usafirishaji wa bidhaa mambo yanayohitaji usalama wa hali ya juu, na kwa kuwa barabara ya Ole Kengeja kuanzia Ole Kianga hadi Kiwani hakuna kituo kidogo cha polisi (police post) hata kimoja.

Je, ni lini Serikali itaamua kujenga angalau vituo vidogo viwili vya polisi katika barabara hiyo vitakavyosaidia hali ya usalama barabarani pamoja na kuzuiya usafirishaji wa mali za wizi kupitia barabara hiyo.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

181. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ni mikakati gani inaendelea kufanyika ili kuzifanya Mahakama zetu kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi.

**Wizara ya Afya:**

164. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Hospitali ya Fuoni inafanya kazi saa 24, na kwa kuwa pesa wanazopata za umeme hazitoshelezi kwa mahitaji ya umeme kwa mwezi, sambamba na hilo Hospitali ya Fuoni Kibondeni haina walinzi kwa muda mrefu sasa licha ya kuwa mna vifaa vya gharama kubwa.

(a) Je, ni lini Wizara itaongeza fedha za umeme katika Hospitali hiyo.

(b) Je, ni lini Serikali itaweka walinzi katika Hospitali hizo za Fuoni na Kibondeni.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

139. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Wananchi wa jimbo la Pandani wanaipongeza Serikali kwa jitihada zake za kuboresha miundombinu na maeneo ya michezo. Hata hiyo, katika jimbo la Pandani, viwanja vizuri vya michezo vimekuwa vikiathiriwa sana na maji na kuvipotezea sifa zake.

(a) Je, ni upi mgawanyo wa majukumu katika kutunza na kukarabati viwanja vya michezo vilivyomo ndani ya jimbo la Pandani.

(b) Je, kwa miaka mitano iliyopita, Serikali imesaidiaje katika

kuboresha viwanja vya michezo vilivyomo ndani ya jimbo la Pandani.

(c) Je, kwa miaka mitano ijayo, Serikali ina mpango gani wa kuboresha viwanja vya michezo vilivyomo ndani ya jimbo la Pandani.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

102. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Kwa nia nzuri Serikali iliamua kuruhusu uchimbaji wa mchanga Shehia ya Shumba Vyamboni katika jimbo la Tumbe.

(a) Je, ni vigezo vipi vilivyotumika katika kuruhusu uchimbaji huo.

(b) Kwa kuwa ni maeneo ambayo yalikuwa yakitumiwa na wananchi kwa shughuli mbali mbali za kujipatia riziki. Je, kuna fidia yoyote waliolipwa wananchi hao.

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

3. MHESHIMIWA NASSOR SALUM ALI (Jimbo la Kikwajuni) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Hivi karibuni kumekuwa na taarifa za matukio ya kuokotwa watoto wachanga wanaotupwa baada ya kuzaliwa. Inaonekana hatua za upelelezi hazifiki mwisho kuwabaini wahusika na kuwachukulia hatua.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna ulazima sasa wa kuweka utaratibu katika shehia na kila nyumba yenye mjamzito itowe taarifa kwa sheha na kuwekwa kumbukumbu.

(b) Je, Serikali haioni ulazima kurekebisha Sheria ya Usajili wa Matukio ya Kijamii na kuwawezesha usajili wa kila ujauzito kwenye Rejista maalumu kupitia kwa masheha kabla usajili wa kizazi.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

185. MHESHIMIWA SHADYA MOHAMED SULEIMAN (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Kina mama ndiyo wenye mzigo mzito kwenye familia na kusababisha kujiingiza kwenye miradi mbali mbali kama kulima mwani lakini bado kina mama hawa wanapoteza nguvu kubwa kuliko kipato.

(a) Je, soko la mwani duniani likoje.

(b) Ni lini Serikali itakamilisha kiwanda cha mwani kilichopo Chamanangwe na kuwaacha kina mama hawa kukaa na mwani majumbani bila kuuzwa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2022/2023.

**Waziri wa Afya:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
16 Mei, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA